



# **KIBABII UNIVERSITY**

## **UNIVERSITY EXAMINATIONS**

**2021/2022 ACADEMIC YEAR  
FIRST YEAR SECOND SEMESTER**

**MAIN EXAMINATION**

**FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)**

**COURSE CODE: SWA 122**

**COURSE TITLE: MISINGI YA FASIHI**

**DATE: 09/05/2022**

**TIME: 9:00AM-11:00AM**

---

**MAELEKEZO**

Jibu maswali matatu pekee.

**MUDA: Masaa Mawili (3)**

**KIBU observes ZERO tolerance to examinations cheating**

## Maswali

1. a) Eleza maana ya fasihi. (alama 2)  
b) Bainisha mitazamo yoyote miwili inayoeleza asili ya sanaa. (alama 6)  
c) Linganisha fasihi andishi na fasihi simulizi kwa kutumia hoja zozote tano. ((alama 10)  
d) Jadili jinsi fasihi inavyoathiri maisha ya mwanadamu. (alama 12)
2. Jadili maudhui yoyote matano yaliyoshughulikiwa katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*. (alama 20)
3. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

### Ua

Natamani kutamka, Mungu unipe karama,  
Nipe karama Rabuka, nilisifu ua jema,  
Lifaalo kusifika, kulisifu huwa vema,  
Mungu nipe baraka, nijale kulichuma.

Lina urembo wa nuru, ua ninalolisema,  
Machoni halidhuru, linavuta kutazama,  
Sana ningeshukuru, kupata ua la kima,  
Kitu kisichodhuru, kukipata ni heshima.

Nataka nilichume, liwe langu ua jema,  
Nilitunze nitazame, nifurahike daima,  
Liwe ngao niegeme, nilifanyie huruma,  
Wenye wivu wasiseme, Baraka imenihama.

Mwenye niamru, niombali liwe tama,  
Ua liwe na uhuru, liishi maisha mema,  
Kisha ulinusuru, mwivi asiye lichuma,  
Upendacho si kufuru, kukiombea mema.

Sauti yangu ifike kwa mgawaji neeme,  
Wanipendao wacheke, wafurahike neema,  
Nakuomba nishike, mkono usende nyuma,  
Ua lisiniponyoke, nilishakapo 'tahema.

Hakufuru mwombaji, ambapo neno jema,  
Muumba ndiwe mpaji, uliyetupa kalmia,  
Makusudi mahitaji, tuyaweze kuyasema,  
Nataka unifariji, wala pasiwe lawama.

### Maswali

- a) Eleza maana ya sitiari ya neno 'Ua' katika muktadha wa shairi hili. (alama 2)
  - b) Eleza muundo wa shairi hili kwa kuzingatia hoja zozote tano. (alama 5)
  - c) Pambanua uhuru wowote wa mshairi kwa kuzingatia hoja zozote nne. (alama 4)
  - d) Liweke shairi hili katika bahari zozote tatu. (alama 3)
  - e) Jadili maudhui yoyote matatu katika shairi hili. (alama 6)
4. Jadili dhamira zozote tano za mtunzi katika tamthilia ya *Mashetani*. (alama 20)
  5. a) Kwa kuzingatia hoja zozote tano, eleza umuhimu wa kufanya utafiti katika utanzu wa fasihi simulizi. (alama 10)  
b) Fafanua changamoto zozote tano ambazo zinaweza kumkumba mtafiti wa fasihi simulizi. (alama 10)